# OFISI YA RAISI-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA

**SHULE YA SEKONDARI UPONERA,**
**S.L.P 33,**
**MAHENGE/ULANGA.**

**Tarehe ..................................**

**Kumb Na.UPSS/ADMIN/VOL.II/2**

Jina la mwanafunzi.........................................
Jina la Shule aliyotoka....................................
S.L.P............................................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UPONERA-WILAYA YA ULANGA MKOA WA MOROGORO-20.....**

## 1.0.UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka wa masomo wa 20.........Shule ya sekondari UPONERA ipo umbali wa kilometa mbili (2), mashariki mwa Halmashauri ya Ulanga na inafikika kwa aina mbalimbali za usafiri toka kona mbalimbali za mji wa Mahenge.

Mwaka wa masomo wa 2020 unaanza tarehe hivyo mwanao anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe hadi na baada ya hapo udahili utafungwa.

## 2.0. MAHITAJI MUHIMU NA VIFAA VYA SHULE

Mwanao ajapo shule atahitajika kuja na:

(A) Sare sahihi za shule ambazo ni: **ni suruali ya kaki iliyokolea, yenye pindo na isiyobana (siyo modo) kwa wavulana na sketi ya khaki inayovuka magoti (ndefu) ya linda box au blauzi nusu kanzu-nyeupe, hijabu nyeupe na suruali ya rangi ya kaki (isiyobana) kwa wasichana.** (upana wa pindo la suruali uwe nchi 16)

(B) Kiatu cheusi chenye kamba (si yebo yebo)

(C) Daftari, zisizopungua tisa kwa masomo tisa yanayofundishwa shuleni. Mzazi anashauriwa kumnunulia mwanae daftari za counter books zinazoweza kudumu kwa muda mrefu.

(D) Kalamu za wino wa bluu au nyeusi au mweusi, kalamu ya risasi, mkebe,rula na ufuto.

(E) Tai rangi ya khaki na ni lazima awe nayo

(F) Sweta la rangi ya kijani kibichi

(G) Soksi nyeupe jozi mbili (2).

## 3.0. SHERIA NA KANUNI MBALIMBALI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978, kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Elimu Na.1995, ya mwaka 1995.

Aidha, shule hii inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wiara ya Elimu, Sayansi-Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi ya Raisi-TAMISEMI, zinazosimamia Elimu nchini.

**3.1.Mwanafunzi akishakubali kujiunga na Shule ya Sekondari Uponera: anatakiwa:**

(A) Kuwa na heshima kwa viongozi,walimu wazazi, wanafunzi wenziwe na jamii ya shule kwa ujumla

(B) Kuwa na mahudhurio mazuri shuleni siku zote za masomo na anapohitajika shuleni, ikiwemo mwisho wa wiki inapobidi

(C) Kuwahi Shuleni na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifu

(D) Kutunza haiba yake kwa usafi wa mwili, mavazi na kutumia lugha yenye staha

(E) Kutunza mali za shule kwa umakini mkubwa wakati wote, la sivyo atazilipa au kufutwa shule

(F) Kuvaa sare za Shule wakati wote akiwa shuleni, isipokuwa kwa ruhusa au shughuli maalumu

(G) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo au kutokuwepo katika eneo la shule

(H) Kupokea na kuwaelekeza wageni kutokana na mahitaji yao mbalimbali wafikapo suleni

(I) Kujiepusha na: kiburi, hasira na kutoa kauli chochezi na kutumia lugha za matusi na zinazoweza kuudhi

**3.2. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

Mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule akifanya au kuhamasisha kufanyika kwa makosa yafuatayo:

(A) Wizi wa mali ya/za shule au ya/za wanafunzi wenzake

(B) Uasherati, usagaji na ushoga

(C) Ubakaji

(D) Ulevi, matumizi,uuzaji au usafikirishaji wa dawa za kulevya kama vile:bangi,kokeni, mirungi, kubeli, shisha,ugoro na uvutaji sigara

(E) Kupigana au kupiga

(F) Kuharibu kwa makusudi mali za umma

(G) Kudharau bendera na picha za viongozi wa taifa

(H) Kupata,kutoa au kusababisha ujauzito

(I) Kugoma,kuchochea, kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au jamii inayoizunguka shule

(J) Kukataa adhabu kwa makusudi

(K) Kukutwa na, au kumiliki simu ya mkononi

**4.0. MAMBO MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI WAKATI WA UDAHILI WA MWANAFUNZI:**

Mzazi unapomleta mwanafunzi shuleni unatakiwa uhakikishe anakuja na:

(A) Hati ya uthibitisho wa hali ya afya ya Mwanafunzi (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na mganga-hospitali ya wilaya-**baada ya vipimo vya afya.**Hii itasaidia uongozi na shule kwa ujumla katika:kugawa kazi na majukumu mbalimbali, kutoa adhabu na maagizo mbalimbali kwa wanafunzi

(B) Maelezo binafsi-yenye ushahidi kuhusu historia ya mwanafunzi na kukiri kuwa mtiifu na kujiepusha na migomo, fujo na makosa ya jinai awapo shuleni.

**NB:Tafadhali soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI UPONERA**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI UPONERA
S.L.P 33. MAHENGE / ULANGA

**Mwl. JANETH C. KANGUSI**

**MKUU WA SHULE**